# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 2

# 83 Maandiko kwa ukuta

### Kwa Biblia

Danieli mlango wa 5

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ana amri juu ya mataifa. Anatimiza kuzudi lake katika ulimwengu. Mungu ataadhibu wale wanaofanyia jina lake madharau

### Somo

Belshaza alikuwa mfalme wa Babeli. Belshaza alikuwa mjukuu wa Nebukadreza. Belshaza alikuwa Mfalme hafifu.

Koreshi alikuwa Mfalme wa Uajemi. Koreshi alikuwa mfalme wa nguvu. Alipigana vita vingi. Alikuwa anajenga ufalme mkubwa. Babeli ilikuwa adui yake ya nguvu sana. Koreshi alitaka kuchukua mji wa Babeli. Koreshi aliendelea kukaribia Babeli. Alipiga kambi karibu na huo mji.

Belshaza hakukuwa na wasiwasi wakati Koreshi alipokuwa akisongea Babeli. Alijiamini kwamba hakuna anayeweza kushinda Babeli. Kuta za Babeli zilikuwa pana na za nguvu. Hazingeweza kubomolewa na yeyote. Mto wa Frati ulipita katikati ya mji wa Babeli. Kulikuwa na maji mengi sana kwa huo mji. Kulikawa na mashamba. Kulikuwa na chakula kingi. Watu wa Babeli waliamini kwamba mji wao ungeweza kuzingirwa hata kwa miaka 100.

Belshaza hakuogopa Koreshi na jeshi lake. Alikuwa anashugulika na kutengeneza karamu kubwa. Belshaza alikaribisha watu elfu moja wa maana kwa karamu yake. Kulikuwa na chakula kingi na mvinyo kwa wingi. Belshaza alichangamka na kufurahia hiyo sherehe kubwa, akiwa na wageni wake wa maana.

## Maswali

1. Nani alitaka kupiga Babeli?
2. Nani alifanya karamu kubwa?
3. Mfalme Belshaza alitumia vikombe gani?
4. Alikuwa akisifu nani alipokuwa akikunywa mvinyo kwa vikombe vya Mungu?
5. Nini ilifanya Mfalme Belshaza akaogopa?
6. Nani aliweza kusoma maandiko yaliyokuwa kwa ukuta?
7. Maandiko yalisema nini? Maandiko yalimaanisha nini?
8. Ujumbe wa Mungu kwa Belshaza ulisema nini?
9. Mfalme Koreshi alifanya mpango gani wa ujusi?
10. Nini ilifanyika usiku huo huo?

## Majibu

1. Koreshi Mfalme wa Uajemi alitaka kupiga Babeli.
2. Mfalme Belshaza alifanya karamu kubwa.
3. Mfalme Belshaza alitumia vikombe vya dhahabu na vya fedha kutoka kwa Hekalu ya Mungu.
4. Belshaza alikunywa mvinyo akitumia vikombe vya Mungu lakini alitukuza miungu ya Babeli.
5. Belshaza aliona mkono ukiandika maneno mageni kwa ukuta.
6. Danieli aliweza kusoma maandiko yaliyokuwa kwa ukuta
7. Mene, Mene, Tekeli, na Peresi. Hesabiwa, hesabiwa, kupimwa na kugawanyika.
8. Utawala wako umegawanyika na umekwisha. Umepimwa na kujulikana uko muovu. Ufalme wako umegawanyika na kupewa Wamedi na Waajemi.
9. Mfalme Koreshi aligeuza Mto wa Frati uteremke upande mwingine.
10. Koreshi aliendea kwa mtaro wa mto uliokauka. Alishinda Babeli. Belshaza aliuawa. Dario alifanywa mfalme. Maneno ya Mungu yalitimizwa kuwa ya kweli.

Mfalme Nebukadreza aliposhinda Yerusalemu, alichukua vikombe vya Mungu vya dhahabu na vya fedha. Nebukadreza alipeleka hivi vikombe Babeli. Belshaza aliamrisha watumishi wake walete vile vikombe vya Mungu vya dhahabu na vya fedha kwa karamu yake.



Belshaza na wageni wake walikunyuia kwa vikombe vya Mungu. Walikuywa mvinyo na kutukuza miungu ya Babeli. Belshaza alikuwa akisema kwamba miungu ya Babeli wanashinda Mungu wa Israeli. Alitumia vikombe vya Mungu na kukunyuia miungu. Belshaza alidharau Jina la Mungu.




Bude si bude vidole vya mkono vilionekana na kuandika kwa ukuta wa nyumba ya kifalme. Mfalme Belshaza aliangalia mkono ulipokuwa ukiandika. Mkono ulitokea pasipojulikana. Uliandika maneno yasiyoeleweka kwa ukuta.

Mfalme Belshaza aliogopa. Uso wake ulibadilika. Magoti yakagongana. Aliogopa mpaka hangeweza kusimama. Mfalme Belshaza alituma waite watu wake wa hekima. Lakini hakuna mtu wake wa hekima aliyeweza kusoma hayo maandiko yaliyoandikwa kwa ukuta. Hapa Mfalme Belshaza aliogopa zaidi.

Malkia alikumbuka Danieli aliyeambia Mfalme Nebukadreza maana ya ndoto yake. Mfalme Belshaza alituma wamuite Danieli. Mfalme aliahidi Danieli zawadi nyingi sana ikiwa atasoma hayo maandiko. Danieli hakutaka zawadi kutoka kwa mtu aliyedharau Jina la Mungu. Lakini Danieli aliambia Mfalme kwamba atasoma maneno yaliyoandikwa kwa ukuta.

Maandiko yalikuwa ujumbe kutoka kwa Mungu. Mungu alikasirika kwa sababu Belshaza alitumia vikombe vya Mungu kuwatukuza miungu wa Babeli. Mungu alikasirika kwa sababu Belshaza alidharau Jina la Mungu. Maandiko yalisema kwamba Belshaza ataadhibiwa kwa sababu ya uovu wake. Maandiko yalisema hivi:

***MeNe MeNe TeKeLi Na PeReSi***

Haya maneno yalimaanisha **Hesabiwa, hesabiwa, kupimwa na kugawanyika**
***MeNe***: Mungu amehesabu siku za utawala wako. Utawala wako umeisha.
***TeKeLi:*** **Umepimwa** kwa kipimio. Wewe ni muovu.
***Na PeReSi:*** Ufalme wako **umegawanyika** na kupewa Wamedi na Waajemi.

Usiku huo huo, Koreshi alikuwa anapanga kushambulia Babeli. Koreshi alikuwa na mpango mzuri sana. Koreshi na jeshi lake walichimba mtaro mkubwa. Walifanya Mto wa Frati eteremke na uelekee upande mwingine. Walizuia Mto kuendea Babeli. Ilipofika usiku, Koreshi na jeshi lake walitembea kupitia kwa mtaro uliokuwa umekauka kutoka kwa maji. Walienda mpaka ndani ya mji. Watu wa maana wote walikuwa na Belshaza kwa karamu yake. Hakukuwa na mtu wa kuwazuia Koreshi na jeshi lake. Wababeli walipatikana bila kujua. Koreshi alishika mji wa Babeli mateka. Mfalme Belshaza aliuawa. Dario Mmedi alitawazwa kuwa Mfalme wa Babeli. Usiku huo maneno ya Mungu yalitimizwa kuwa kweli.

